



JARIBIO LA MTHANI

DARASA LA TANO – 007

KISWAHILI: LUGHA

Muda: Saa 1 Dak. 40

Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 – 15. Kwa kila nafasi umepewa malibu manne. Chagua jibu lillo sahihi.

Maria binti wa miaka ___1___ ambaye ___2___ kwenda shuleni anajua kwa ___3___ kuwa jimbi huwika mara mbili kabla ya ___4___. Anao ujuzi huu kwa sababu inampasa kila siku ___5___ kwenye kibarua chake ___6___ ya jogoo wa pili wa jirani yake kuwika mara ya pili

Kazi yake ___7___ ni kusafisha mapipa yaliyopikiwa pombe ya kienyeji. Kwa sababu ___8___ yeye hucheleva mara kwa mara kufika kazini. Haya hutokea ___9___ ya kulala akiwa amechelewa sana. Ama kweli ___10___ majuto ya Firauni.

1. A. kumi na mbili B. mikumi na mbili C. kumi na miwili D. mikumi na miwili
2. A. hakubahatishwa B. hakubahatisha C. alibahatika D. hakubahatika
3. A. yakini B. yamkini C. lakini D. walakini
4. A. kulala B. kuamka C. kuchwa D. kupambazuka
5. A. kukimbiza B. kukimbilia C. kukimbizwa D. kukimbiliana
6. A. badala B. bila C. kabla D. bali
7. A. huwa B. ilikuwa C. haikuwa D. hakuwa
8. A. ziepukikazo B. ziepukwazo C. ziepukazo D. zisizoepukika
9. A. licha B. baada C. minajili D. fauka
10. A. atajuta B. hujuta C. alijuta D. amejutika

Wakati ___11___, mwajiri ___12___ huwa mkali sana kwake. Yeye hudhania kuwa Maria ni mvivu wakati anapocheleva kufika ___13___. Hata hivyo, ___14___ cha Maria kucheleva huwa ni uchovu ___15___ kutokana na kazi azifanyazo.

11. A. nyingine B. mingine C. kwingine D. mwingine
12. A. yake B. lake C. wake D. chake
13. A. shuleni B. kazini C. skulini D. maabarani
14. A. chanzo B. sababu C. lawama D. uwezo
15. A. nyingi B. jingi C. mwingi D. mingi

Kutoka swali la 16 – 30, jibu kila swali kulingana na maagizo

16. Andika kwa umoja:

- Meko zile zimewakishwa.
A. Meko ile imewakishwa
B. Majiko yale yamewakishwa
C. Jiko lile limewakishwa
D. Jiko zile zimewakishwa

17. Kanusha:

- Kula chakula haraka.
A. Usile chakula haraka.
B. Hujakula chakula haraka.
C. Usikule chakula polepole.
D. Hutakula chakula haraka.

18. Kamilisha methali:

- Haba na haba
A. humaliza gogo
B. hujaza kibaba
C. humaliza buyu
D. ndio mwendo

19. Chagua jibu sahihi:

- Tunda _____ ni tamu sana.
A. hii B. hiyo
C. hiki D. hili

20. Andika tarakimu kwa maneno:
969

- A. Mia tisa na tisini na tisa
B. Eflu tisa na sitini na tisa
C. Mia tisa na sitini na tisa
D. Mia sita na tisa

21. Chagua jibu sahihi kisarufi:

- Nyinyi _____ wali kwa kitoweo.
A. hawali B. hamli
C. hamkuli D. hauli

22. Tegua kitendawili kifuatacho:

- Agnes maridadi.
A. kipepeo B. malaika
C. kifagio D. nyota


23. Jibu salamu ifuatayo:

Hujambo?

- A. Mzuri
C. Salama

- B. Njema
D. Sijambo

24. Jina la umbo lifuatalo ni:



- A. mraba B. mche
C. pembe tatu D. duara dufu

25. Chombo cha jikoni kinachotumiwa kukunia nazi huitwa

- A. mbuzi B. seredani
C. buli D. kinu

26. Tumia kiulizi 'pi' ipasavyo:

Tutakula chakula _____ ?

- A. kipi B. ipi C. zipi D. vipi

27. Aina ya jiko la makaa la kuwekea buli huitwa

- A. jokovu B. chano
C. seredani D. mbuzi

28. Mkulima anapopalilia mimea shambani huwa anafanya kitendo gani?

- A. Kuchipua miche
B. Kung'oa magugu
C. Kunyunyizia maji
D. Kupanda mbegu

29. Chagua sifa inayofaa kujaza pengo: Mwanafunzi huyo ni _____ wa maneno

- A. nyepesi B. jepesi
C. chepesi D. mwepesi

30. Katika wakati uliopita, kitenzi 'anacheza' ni

- A. atacheza B. amecheza
C. alicheza D. hucheza

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 – 40

Baada ya safari ndefu kwenye kijito cha maji yenye mzizimo chini ya mlima, hapo tulikoga na kula mlo wa mchana. Tulipumzika kivulini mwa mti mrefu kwa vile jua lilivyokuwa kali mno.

Baada ya kupumzika, tuliendelea na safari yetu wakati wa alasiri. Tulipanda na kushuka milima mwendo wa aste aste kwani milima ilizidi kuwa mirefu. Tulifika kwenye vilele na vilelecha vya milima wakati wa jua kuaga miti. Tulifanya kambi yetu kwenye pango lililokuwa ndani ya mwamba mkubwa, palikuwa pahali pazuri pa kujilinda na kujikinga.

Ilipofika usiku, tulikoka moto nje ya pango hilo ili kuwaogofya wanyama wakali. Tulikula chajio na kuanza kupumzika. Tulipokuwa tukipumzika, tuliimba nyimbo tamu kama halua ya lozi za kutuongoa. Tulifanya hivi ndipo tusahau taabu na mashaka ya safari yetu.

Aidha, tulimshukuru Maulana kwa kutulinda na hatari zote. Baadaye, tulilala fo! fo! fo! mpaka wakati wa kokoiko za jimbi.

Asubuhi na mapema, tuling'oa nanga tena kuelekea upande wa Kaskazini ya miima. Matumaini yetu yalikuwa ni kufikia ziwa la maji ya chumvi. Ilipofika saa sita za mchana, tukalifikia ziwa lile. Na huo ukawa ndio mwisho na hatima ya safari yetu.

- | | |
|---|---|
| <p>31. Wasafiri walifika kwenye kijito chenye
A. maji ya mzizimo B. maji moto
C. maji baridi D. mlima moto</p> <p>32. Ni jambo gani ambao halikufanyika wasafiri walipofika kijitoni?
A. Walioga miili yao
B. Walikula chakula
C. Walipumzika kivulini
D. Walikoka moto</p> <p>33. Baada ya kupumzika wasafiri waliendelea na safari yao wakati wa
A. alasiri
B. magharibi
C. aduhuri
D. alfajiri</p> <p>34. Kwa sababu ya miima kuzidi kuwa mirefu, wasafiri walisafiri
A. mwendo wa kikombe
B. mwendo wa haraka
C. mwendo wa polepole
D. mwendo wa kukurukakara</p> <p>35. Wasafiri walifanya kambi kwenye pango lililokuwa
A. chini ya jiwe kubwa
B. ndani ya jiwe kubwa
C. ndani ya mwamba mkubwa
D. chini ya mwamba mkubwa</p> | <p>36. Baada ya kukoka moto nje ya pango, wale wasafiri
A. walikula chakula cha mchana
B. walianza kuogopa wanyama
C. walilala fofofol
D. walikula chakula cha jioni</p> <p>37. Ili kusahau taabu za safari, wasafiri
A. walikula chakula kitamu sana
B. walipumzika na kulala kabisa
C. waliziimba nyimbo nzuri nzuri
D. walikuwa halua za lozi</p> <p>38. Wasafiri walimshukuru nani kwa kuwalinda na hatari zote?
A. Fualata B. Mungu
C. Mungwana D. Jimbi</p> <p>39. Wasafiri walitoka upande gani kuelekea mlimani?
A. Kusini ya mlima
B. Magharibi ya mlima
C. Mashariki ya mlima
D. Kaskazini ya mlima</p> <p>40. Kichwa ambacho kinafaa zaidi habari hii ni
A. Mto wa maji ya chumvi
B. Pango lenye wanyama
C. Hatima ya safari
D. Safari yenye shida</p> |
|---|---|

Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 41 hadi 50

Mshike! Mshike! Sauti ya Mzee Kusudi iliongoza wengine. Chazumbe alichomoka kwa wepesi kama umeme. Alikuwa keshapiga kona na kutokomea ughaibuni. Mbio alizokuwa nazo siku hizo zingetosha kujishindia medali ya dhahabu kama angeshiriki

katika kinyang'anyiro cha olimpiki. Katika kuchana mbuga huko, aliteleza na kuanguka chini pul! Hakutaka kuendelea, bali alijiburuta hadi kichakani na kujificha. Alitazama damu ilivyochuruzika chiriri kwenye goti lililochumbuka.

"Mimi siwezi kukubali aibu sampuli hii. Mwana nimezaa leo aje aniasi hivi?" Mzee Kusudi alifoka huku akiongozana na umati wa watu kumsaka bintiye. Aliendelea kutoa cheche za maneno, "Naye aombe nisimtie mkononi, atakiona cha mtema kuni". Huku akinena na kutoa sauti kama gari bovu linalokwea mlima, alitamka, "Leo atanijua kuwa mimi sikuzaliwa juu ya mti!"

Chazumbe aliyasikia yote hayo. Alifikiria sana ndoto iliyotokea muda mfupi kabla ya hapo, ilikuwa kama jinamizi. Ndoto hiyo ilifanana sana na yaliyokuwa yakitokea.

- | | |
|---|--|
| <p>41. Chazumbe alichomoka kama umeme kwa nini?
 A. Alikuwa akimtoroka babake
 B. Alikuwa mchawi
 C. Alikuwa akimhepa mamake
 D. Alikuwa akitoroka viboko vya mwalimu</p> <p>42. Mzee Kusudi alikuwa
 A. askari
 B. mzazi wa Chazumbe
 C. mpita njia
 D. jirani wa Chazumbe</p> <p>43. Maana ya <u>kuchana mbuga</u> ni
 A. kutoka kasi
 B. kukata miti
 C. kuharibu mbuga za wanyama
 D. kuwa wa mwisho kwenye mbio</p> <p>44. Sauti 'Mshike! Mshike!' ilitolewa na nani?
 A. Kusudi
 B. Watoto wa mtaa
 C. Umati wa watu
 D. Chazumbe</p> <p>45. Mbio za Chazumbe zilimletea madhara ya
 A. aibu
 B. kuchumbuka
 C. homa
 D. kushikwa na kupelekwa jela</p> | <p>46. Nani alisema maneno haya, "Leo atanijua kuwa mimi sikuzaliwa juu ya mti"?
 A. Chazumbe
 B. Mzazi wa Chazumbe
 C. Jirani wa Chazumbe
 D. Mpita njia</p> <p>47. Maana ya neno 'sampuli' ni kwa mujibu wa taarifa ni
 A. aina
 B. maneno
 C. kipawa
 D. ajabu</p> <p>48. Kuchomoka kwa wepesi kama umeme kuna maana gani?
 A. Kutembea polepole
 B. Kukimbia sana
 C. Kulala sana
 D. Kujikokota kivivu</p> <p>49. Chazumbe alipoanguka aliumia wapi?
 A. Mkono
 B. Macho
 C. Goti
 D. Shingo</p> <p>50. Kichwa mwafaka cha makala haya ni
 A. Mzee Kusudi
 B. Chazumbe na mbio
 C. Kuchana mbuga
 D. Ndoto ya ajabu</p> |
|---|--|